**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 30.

2. Katika karatasi ya majibu, hakikisha umeandika:-

*(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako* *iii). Nambari ya KNEC*

***Muda:Saa 1 Dak 40***

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 1 hadi 5**

***( Ni asubuhi. Mzee Malema amemtembelea rafikiye Riziki nyumbani mwake. Riziki ameketi chini ya mti)***



**Malema:** Sabalkheri sahibu? Unaendeleaje?

**Riziki :** ***(Akishikilia kifua)*** Alkheri kaka.
Niko salama japo nahisi maumivu mwilini.
Hali ya kwako vipi?salmini. Kwani nini mbaya na wewe?

**Malema:** Niko salama salmini. Kwa nini mbaya na wewe?

**Riziki :** ***(Kwa tabasamu hafifu)*** Sina mabaya ila nahisi kwamba sina nguvu mwilini.

**Malema:** ***(Kwa unyenyekevu)*** Inaonekana kuwa hutilii maanani mambo ya afya yako. Je, unafanya mazoezi kila siku?

**Riziki :** ***(Akitikisa kichwa)*** Unayoyasema ni kweli ndugu yangu. Huwa sifanyi mazoezi.

**Malema:** Unapaswa kujua kwamba mazoezi ya mwili huimarisha afya ya akili

**Riziki :** Ni kweli, ninakubaliana nawe huwa sifanyi mazoezi. Basi unanishauri nifanyeje?

**Malema:** Unachohitajika kufanya ni kuwa unapoamka asubuhi na jioni baada ya kuanza kazi unaweza kujiunga na sisi uwanjani tukimbie tukifanya zoezi. Zaidi ya hayo, usisahau kula chakula chenye virutubishi.

**Riziki :** Ninashukuru kwa mawaidha hayo uliyonipa. Tafadhali nipe muda niyatelekeze. Tukaribie ndani ya nyumba tukale kishuka .

1. Mazungumzo haya yanafanyika wapi?
   A. Uwanjani B. Darasani
   C. Sokoni D. Chini ya mti
2. **"Sabalkheri"** ni salamu za wakati upi?
   A. Wowote B. Asubuhi
   C. Jioni D. Mchana
3. Ifuatayo ni mifano ya mazoezi isipokuwa
   A. kula B. mbio
   C. kuruka kamba D. mchezo wa kandanda
4. Mazoezi husaidia vipi?
   A. Kuzembea sana
   B. Kula sana
   C. Kuimarisha afya ya akili
   D. Kulala sana
5. Kisawe cha **kishuka** ni
   A. chajio B. staftahi
   C. chamcha D. kisebeho

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 6 hadi 10.**

Katika kijiji kidogo cha Baiaa, wanafunzi wa gredi ya sita walikuwa wakijitahidi kujiandaa kwa mtihani wa mwisho wa muhula wa pili. Miongoni mwao alikuwapo Asha, msichana mwerevu na mwenye ndoto kubwa ya kuwa daktari. Siku moja, alikutana na mwanamume mgeni aliyekuwa amevaa vizuri na kuonekana karimu. Alijitambulisha kama "Mjomba Sam" na kudai kuwa anatoa misaada kwa watoto wanaofanya vizuri shuleni. Alimwahidi Asha kwamba angewapeleka jijini kwenye shule nzuri yenye vifaa vya kisasa bila kutozwa malipo yoyote.

Asha alivutiwa sana, lakini alipoeleza rafiki yake Halima, Halima aliwajuza walimu jambo hilo nao wakachukua hatua ya haraka. Ilibainika kuwa "Mjomba Sam" alikuwa mlanguzi wa watoto, aliyejifanya mfadhili ili kuwanasa watoto wadogo kwa ahadi za uongo. Shukrani kwa ujasiri wa Halima na walimu wa shule. Asha na wanafunzi wengine waliokolewa kabla hawajanaswa. Wanafunzi walifundishwa jinsi ya kujitambua, kuuliza maswali na kutowaamini watu wasiowajua hata kama wanaonekana wema. Walijifunza pia kuwa kamwe wasikubali zawadi au safari kutoka kwa watu wasio na uhusiano na wazazi au walimu wao.

Tangu siku hiyo, kijiji cha Balaa kilianzisha kampeni ya uhamasishaji dhidi ya ulanguzi wa watoto, na shule ikawa sehemu salama zaidi kwa kila mwanafunzi. Asha aliendelea kusoma kwa bidii, akiwa mfano wa kuigwa na onyo hai dhidi ya hatari ya kuamini njia za mkato za kufikia mafanikio maishani.

6. Asha alikuwa mwanafunzi wa gredi gani?
   A. Nane B. Saba
   C. Tano D. Sita

7. Asha alikuwa mwanafunzi wa aina gani?
   A. Aliyetazamia kujiunga na gredi ya kumi
   B. Mwenye mawazo na matamanio makubwa maishani
   C. Mwenye kurukia mambo bila kuyachunguza
   D. Aliyependa kukaa upweke bila marafiki

8. Mwanafunzi anayejithamini ana tabia zote hizi ila;
   A. kupendelea kujificha nyuma ya makundi mabaya
   B. kutia bidii shuleni bila kulazimishwa
   C. kuiyakataa mambo yoyote yawezayo kumharibia ndoto yake maishani
   D. kuwa na heshima kwake na kwa wengine

9. Kulingana na mwalimu, ukomavu wa mwanafunzi unaonekana pale ambapo
   A. anaendeleza kujiamini mwenyewe
   B. anakuwa na moyo mgumu
   C. anajithamini kwa mafanikio ya maisha yake
   D. anajikosoa badala ya kujisikitikia na kujionea huruma

10. Mwandishi anamalizia kwa kusema kuwa msingi wa mafanikio maishani ni
    A. kujirekebisha B. kutojisikitikia
    C. kutia bidii D. kujithamini

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 11 hadi 15.***

Siku moja Fisi alikuwa matembezi alipita njia iliyopakana na msitu mkubwa fisi alihisi njaa kweli kweli. Kwa muda wa juma moja hakuwa amekula chochote. Tumbo lake lilinguruma ngrr!!! ngrr!!! . Alipofika penye daraja alikula miayo kisha akavuka daraja. Jasho lilimtoka na mwili ulimtetea kwa uchovu. Chini ya mlima, upande wa pili alipata njia moja ilielekea kwenye makazi ya simba, nayo ile ingine ilielekea penye makazi ya sungura. Ghafla, fisi alikuwa akihema, alihisi harufu nzuri ya mchuzi rojorojo. Mate yalimtiririka tiriri, alishindwa atafuata njia gani.

Alipoifuata ya kwanza alirudi. Alijaribu ya pili lakini akarudi. Nia yake ilikuwa kupata mchuzi ulionukia kabla ya mnyama yeyote yule. Aliuweka mguu mmoja kwenye njia iliyoelekea kwa simba kisha ule mwingine ukakanyaga ile iliyoelekea kwa sungura. Kadri fisi mlafi alivyoenda ndivyo miguu yake ilivyozidi kupanuka. Hatimaye fisi mlafi alipasuka msamba, akaanguka chini kwa kishindo na kwenda jongomeo.

11. Fisi mlafi alikuwa amekaa siku ngapi bila chakula?
    A. Siku saba
    B. Siku tano
    C. Siku nyingi
    D. siku moja

12. Tumbo la fisi lilinguruma ngrr!! ngrr!! hiyo ni fani gani ya lugha?
    A. Tashbihi
    B. Msemo
    C. Fumbo
    D. Tanakali ya sauti



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

13. Fisi ni sawa na
A. Bakaye B. Mbwa
C. Uchoyo D. Furaha

14. Alipofika penye daraja kabla ya kuruka, fisi alifanya nini?
A. Aliomba B. Aliona njaa
C. Alikula kidogo D. Alikula miayo

15. Kwa nini tumbo la fisi lilinguruma?
A. Alikuwa amekaa kwa muda wa wiki moja msituni
B. Hakuwa na chochote ndani yake
C. Alihisi njaa kwa muda wa wiki mzima
D. Alihisi kuchoka baada ya karamu

***__Soma kifungu kifuatacho kina nafasi 16 hadi 20. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.__***


Baada ya siku ____**16**____ kupita, wakao na kisiwa____**17**____ mbali, wakakusudia kwenda ____**18**____. Walipokaribia, wakaona ____**19**____ moja zuri lakini hakukuwa na ____**20**____ yoyote ya watu.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **16.** | A. wingi | B. nyingi | C. mengi | D. wengi |
| **17.** | A. na | B. ya | C. kwa | D. cha |
| **18.** | A. kuitazama | B. kutazama | C. kukitazama | D. kupatazama |
| **19.** | A. jumba | B. chumba | C. nyumba | D. vyumba |
| **20.** | A. dalali | B. dalili | C. dhalili | D. adili |

**__Kutoka swali la 21 hadi 30, chagua jibu sahihi kulingana na maagizo uliyopewa.__**

21. Jibu la "**Alamsiki**" ni
A. Binuru B. Marahaba
C. Tunayo D. Nawe pia

22. Sehemu hii ya mwili huitwa aje?



A. Taya B. Goti
C. Kisigino D. Muundi

23. Pete ni aina ya pambo ambalo huvaliwa,
A. shingoni B. sikioni
C. kidoleni D. kichwa

24. Nomino '**chawa**' iko katika ngeli gani?
A. I-ZI B. A-WA
C. LI-YA D. KI-VI

25. **Kamilisha methali ifuatayo.**
Penye moshi hapakosi
A. kuni B. wapishi
C. hatari D. moto

26. Shada ni kwa maua kama vile ____________ ni kwa askari.
A. kikosi B. thurea
C. mlolongo D. kilinge

27. **Tegua kitendawili hiki.**
Anakuangalia tu wala halali au kutembea.
A. jua B. picha
C. jicho D. kioo

28. **Chagua wingi wa sentensi hii.**
Ugonjwa huu ni hatari.
A. Magonjwa hayo ni hatari
B. Ugonjwa huu ni hatari
C. Magonjwa haya ni hatari
D. Magonjwa hizi ni hatari

29. Chagua kifaa ambacho hutumiwa na fundi kushona nguo.
A. Pima maji B. Pima joto
C. Randa D. Cherehani

30. **Chagua ukanusho wa;**
Wewe umekuja kuniona.
A. Wewe hujaja kuniona
B. Wewe haujaja kuniona
C. Wewe hujakuja kuniona
D. Wewe haujakuja kuniona



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

## Sehemu ya B: INSHA

| JINA LAKO | |
|---|---|

**Mwandikie rafiki yako anayosoma katika shule ya malazi barua ukimwelezea jinsi unavyoendelea.**



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com